**Maswali na Majibu**

1. Jiwe kubwa lenye Yoshua aliweka juu liliwakumbusha watu nini?
   *Kwamba walikuwa wameahidi eti watampenda na kumtii Mungu*.
2. Kila kabila ilitakiwa kufanya nini kwa watu waovu walioishi kwa nchi yao?
   *Walikuwa wawaangamize.*
3. Nani angewasaidia kuangamiza wale watu?
   *Mungu angewasaidia kama wangekuwa na imani.*
4. Nini ilifanyika Waisraeli walipopenda na kumtii Mungu?
   *Mungu aliwabariki wawe na mavuno mazuri na kuwapa amani.*
5. Nini ilifanyika Waisraeli walipomwacha Mungu na kuabudu sanamu?
   *Mungu aliwaadhibu kwa kuwaletea njaa na maadui kuwashambulia*.
6. Mungu alituma nani kusaidia Waisraeli walipomgeukia?
   *Mungu alituma waamuzi kuwaokoa kutoka kwa maadui.*
7. Waamuzi walitawala kwa muda gani? *Karibu miaka 400*
8. Debora na Baraka waliwaangamiza Wakanaani namna gani?
   *Mungu alituma dhoruba kubwa mpaka magari ya Wakanaani yakagwama kwa matope*
9. Mbona Samsoni alikuwa na nguvu sana? Aliwaua Filisti namna gani?
   *Hakuwahi kunyoa nywele yake. Aliangusha hekalu juu yao*.
10. Nini inaweza kufanyika kila mtu akifanya kinachopendeza macho yake?
    *Kunakuwa na fucho, jeuri, uovu na mateso*

## Mistari ya kukariri

Waamuzi 21:25 Yakobo 4:4

## Mazungumzo

Mbona liwe jambo la maana kutii amri za Mungu? Nini itafanyika ikiwa tutajipenda sisi wenywe? Mungu alisaidia Waisraeli namna gani walipokuwa wakiteswa? Mungu anatusaidia namna gani tukimrudia?

## Kuandika

Eleza vile Mungu alisaidia Waisraeli kupitia kwa Gideoni na watu wake 300.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 18 Wakati wa Waamuzi

**SOMA Waamuzi 1:19 na 27 – 33; Waamuzi 21:25; Waamuzi 7:19 – 22**

**SOMO**

Yoshua alipokuwa mzee sana, aliita watu wote ili wakutane naye kule Shekemu. Aliwakumbusha miujiza yote yenye Mungu aliwafanyia. Aliwakumbusha vile Mungu alikuwa amewapa Nchi ya Ahadi.

Yoshua aliwakumbusha kwamba Mungu aliwachagua kama watu wake wa kipekee. Wakimtii Mungu, atawabariki katika hiyo nchi. Ni lazima wajitenge na watu wa hiyo nchi - wasioe watu wa huko au wasiabudu sanamu zao. Wasipomtii Mungu, atawaadhibu - kutakuwa na njaa kwa nchi yao na maadui watakuja na kuwapiga.

Yoshua aliwambia kwamba lazima waamua kama watampenda Mungu na kutii amri zake. Watu waliahidi kupenda na kutii Mungu na kukumbuka upendo wake wote kwao. Yoshua aliandika makubaliyano hayo yote kwa kitabu, akachukuwa jiwe kubwa kule Shekemu halafu akaweka ili liwe ukumbusho kwao. Halafu Yoshua akafa akiwa na umri wa miaka 110. Punde si pumde watu walisahau ahadi yenye walifanya.




Yoshua aliongoza Waisraeli kuingia kwa Nchi ya Ahadi. Walikuwa wameharibu miji na kuvunja nguvu ya mataifa yaliyokuwa yakiishi huko. Yoshua alikuwa amegawa kila kabila mahali pao pa kuishi. Ilikuwa juhudi za kila kabila kumalishisha kuwaondoa wale watu waovu waliokuwa bado kwao.

Mungu alikuwa amewambia kuharibu watu wote waovu waliokuwa wakiabudu sanamu. Kila kabila ilikuwa imalize kuwaangamiza kwa sehemu yao. Kama wangetii Mungu, hakungekuwa na sanamu kwa nchi yao. Waamuzi 1:9 inatwambia kwamba Yuda hawakufukuza watu wote eti kwa sababu walikuwa na magari ya chuma. Hii ni kwa sababu watu wa Yuda hawakuwa na imani kwa Mungu. Kama wangeamini Mungu wangepiga na kuharibu adui wao wote. Waamuzi 1:27 – 33 ni huzuni kwa sababu hata kabila za Israeli wote hawakutii Mungu na kuwaondoa hao watu waovu na sanamu zao.

Waisraeli hawakuchukuwa nchi yote. Badala yake walifanya urafiki na watu wa kule na wakaanza kuabudu sanamu kando na Mungu. Wakati wa waamuzi mambo yaliendelea kujirudia. Kwanza Mungu alituma waamuzi kufundisha Waisraeli sheria zake. Walipopenda Mungu na kumtii, aliwabariki wakawa na mavuno mazuri na kuiishi kwa amani.

*Dagoni*





*Baali*

Waisraeli waliendelea kufanya urafiki na watu waovu waliobaki kwa nchi. Walianza kuabudu sanamu zao – Baali, Dagoni na Ashterothi. Walipomwasi Mungu, aliwaadhibu – kulikuwa na njaa nchini na maadui waliwapiga. Waisraeli walipokuwa na shida kutoka kwa maadui wao, walimrudia Mungu tena. Mungu aliwatumia waamuzi kuwasaidia na kuwarudisha kwa Mungu na kuwafunza njia zake. Huu mtindo uliendelea kwa miaka 400. Kwa huo muda, waamuzi 12 waliwafunza Waisraeli juu ya Mungu na kuwaokoa kutoka kwa maadui.

*Ashterothi*



Kuna wakati Waisraeli walimwacha Mungu na Wakanaani wakawaongoza kwa miaka 20. Baadaye wakarudia Mungu awasaidie. Mungu alituma Debora nabii wa kike ili awe mwaamuzi. Aliendа na Baraka kupigana na Wakanaani. Baraka alikuwa na watu 10,000 na magari 900 ya chuma kwenda kupigana na Wakanaani maelfu. Mungu alituma dhoruba ya ajabu na magari ya Wakanaani yaligwama kwa matope. Jeshi la Kanaani lilitoroka. Mungu aliwafanyia Waisraeli ushindi mkubwa na hapo walitii na kuwa na amani kwa miaka 40.

Baadaye Waisraeli waliacha Mungu tena. Wamidiani waliwatesa na kufanya maisha yao kuwa ya taabu. Walipogeukia Mungu awasaidie, Mungu alichagua Gideoni awe mwaamuzi wao. Gideoni alikuwa na watu 300 pekee kupigana na jeshi la Wamidiani waliokuwa wengi hawangesabuliwa. Mungu aliambia Gideoni agawanye watu wake kwa vikundi vitatu. Kila mtu alikuwa na tarumbeta na mwenge wa moto ndani ya mtungi. Usiku ulipofika vikundi vyote kando ya kambi ya Wamidiani. Walizivunja mitungi zao, wakaenua juu mienge za moto na kupiga tarumbeta. Walitoa sauti za juu wakisema. “Upanga wa Mungu na wa Gideoni.” Wamidiani waliamka kwa uoga.



vilizingira Walichanganyikiwa na kuanza kupigana wenyewe kwa wenyewe wakitoroka. Kwa hivyo Mungu aliletea Waisraeli ushindi mwingine.

Baadaye Waisraeli waliacha Mungu tena. Wafilisti wakawatesa kwa miaka 40. Walipomliliia Mungu awasaidie, Mungu aliwaletea Samsoni awe mwaamuzi wao. Mungu alisema kwamba lazima Samsoni asinyoe nywele na Mungu alimpa nguvu nyingi ya kupigana na Wafilisti. Lakini Samsoni alimwambia mwanamke Delila sababu ya nguvu zake. Delila alimnyoa Samsoni nywele yenye ilikuwa uwezo wa nguvu zake. Kwa hivyo walimshika Samsoni na kumtoa macho halafu wakamweka gerezani. Nywele za Samsoni zilipokua, Samsoni aliomba Mungu ampe nguvu tena na aliangusha hekalu na Samsoni akafa na watu 3,000. Halafu Mungu akawezesha Waisraeli kuwa na ushindi na amani tena.

Mstari wa mwisho wa kitabu cha Waamuzi unazungumzia kwamba Waamuzi hawakuwasimamia Waisraeli tena, “Wakati huo hakukuwa na mfalme katika Israeli. Kila mtu alifanya kilichompendeza.” Amri za Mungu zinaleta amani na uhaki, lakini kila mtu akifanya vile anapenda, kutakuwa na fucho, jeuri uovu na mateso. Haya ndiyo yalifanyika wakati wa waamuzi.

Kulikuwa na wakati Waisraeli waligeukia Mungu. Alikuwa akiwapea mwamuzi na alikuwa anawaokoa kutoka kwa maadui na kuwarudisha kwake.